

Ulinzi wa makanisa katika uisilamu

Kimetolewa

Na

Profesa \ Mohammed Mukhtar Juma

Waziri wa Wakfu wa Misri

Profesa \ Shauky Alaam

Mufti wa Misri

Kimefasiriwa

Na

Profesa \ Ayman Ibrahim Al aasar

Kitivo cha lugha na ufasiri

Kairo 1437 H / 2016 AD

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

Zawadi

kwa

Mheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya watu wa Misri/ Abdul Fatah Al-Sisi, Mwenyezi Mungu akuhifadhi. Kutokana na juhudi zako kubwa za kupambana na ugaidi na misimamo mikali duniani na kwa kuheshimu muono wako wa utamaduni katika kurekebisha hotuba za kidini. Na katika utekelezaji wako katika kutilia mkazo fikira za wastani na kurenda katika kuinua misingi ya kuishi kwa amani kwa walimwengu wote. Kwa haya yote, tuna furaha kukupa zawadi kitabu hiki ambacho hutolewa na Wizara ya Wakfu kikiwa na malengo ya kurekebisha ufahamu potofu na wenye makosa na kudurusu matukio mapya ya kisasa kwa mtazamo wenye kuchunga uhalisia na kuelezea uhakika wa uisilamu mtukufu na ustaarabu wake wa kiutu.

Utangulizi wa kitabu kwa waandishi wake

Neno la Waziri wa wakfu

Dibaji

Shukurani zote njema ni za Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu wote, rehema na amani zimshukie Mjumbe Mtume wa mwisho Muhammad Bin Abdillah na watu wake na Masahaba zake na kila waliomfuata mpaka siku ya mwisho.

Baada ya utangulizi.

Kutokana na imani yetu juu ya umuhimu wa kuwepo marekebisho ya hutuba za kidini, na kudurusu kwa undani kabisa matukio mapya yanayozuka hivi sasa, na kuuweka wazi msimamo wa dini yetu tukufu kwa walimwengu, na kuyakabili matatizo makubwa kwa hekima na ushujaa kwa kupitia wasomi na maulamaa walio na ujuzi thabiti.

Na kuiweka wazi misingi ya dini kwa walimwengu pasi na kubagua, na kuendeleza mwenendo wa kuishi kwa pamoja na kushirikiana kwa pamoja kati ya walimwengu bila ya kubaguana kwa misingi ya kidini, rangi, ukabila, utaifa na lugha..

Hii ni kutokana na imani yetu na kama ilivyo katika maneno ya Mwenyezi Mungu { **Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.** } (Albaqara; 256}. Ama kuhusu kutafautiana kwa walimwengu ambayo ni mwenendo (kawaida) wa kiulimwengu Mwenyezi Mungu anasema {Na Mola wako Mlezi angelipenda angewafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitalifiana, Isip kuwa wale ambao Mola wako Mlezi amewarehemu; na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu amewaumba. }(Hud;118-119).

Na kuepukana na mtazamo finyu wa kimawazo na kuelekea katika mtazamo mpana wa kiisilamu na kuheshima pande nyengine, na kutokna na pupa ya kudhihirisha ukweli kwa wengine kwanza lazima tuwe wakweli wa nafsi zetu, na kuenda sambamba na misingi ya kukubali na kuheshimu mawazo ya mwengine, na kukana fikira za siasa kali na kuuhakikishia ulimwengu wote juu ya ubora wa dini ya kiisilamu na yanayojiri ndani yake ni jaribio la kuuchafua ambayo hayana uhusiano au ilaka yoyote katika dini hii. Kwa ajili hiyo, kitabu hiki “ Ulinzi wa Makania katika Uisilamu” kimechapishwa kwa kuandaliwa na wasomi na maulamaa wenye vipaji na mwisho kupitiwa na mwanazuoni Profesa Shauky Allaam Mufti wa Misri. Na hii ni kwa sababu ya kutaka kwetu kuzungumzia matukio tofauti ya kisasa kwa mlolongo wa vitabu vya kurekebisha ufahamu potofu ambavyo hutolewa na Baraza Kuu la Mambo ya Kiisilamu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwafikishe na kutukubalia kwani yeye ni Mweza juu ya hili. Mwenyezi Mungu ndiye anayejua lengo kusudiwa Naye ni Mwenye kuongoa.

Profesa; Muhammad Mukhtar Juma Mabruk

Waziri wa Wakfu

Mwanachama wa baraza la utafiti wa kiisilamu.

Mkuu wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiisilamu.

Neno la Mufti wa Misri

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

Shukurani zote njema ni za Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu wote, rehema na amani zimshukie Mjumbe Mtume na waliomfuata.

Baada ya utangulizi.

Hakika ujumbe wa kiisilamu unaandamana na maadili ya juu yanayoshikamana na sheria yote kiukamilifu, ni rehema kwa viumbe wote wa Mwenyezi Mungu, na hivi ni kama ilivyoeleza Qurani Tukufu, kwa kufupisha ujumbe huu wa Mtume, ikasema Qurani Tukufu { Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote. }(Alanbiyaa;107). Rehema ni upeo wa juu kabisa wa maadili ambayo hotuba za kiisilamu na itikadi zake na sheria zake zimeambatanishwa hapo.

Kwa ajili hiyo, uisilamu unafaa kwa zama na nyakati na kwa watu na hali, na pia mwingiliano upo wazi kabisa kwa ajili ya kuelewa tamaduni, ustaarabu na kutendana pamoja na dini tofauti hali ya kuhifadhi uasili wa uisilamu na kuheshimu mambo muhimu ya tamaduni na ustaarabu. Dini ni zaidi ya ufahamu wa madhehebu yote, ni rehema za Mwenyezi Mungu ambazo zimeenea kwa wote.

Qurani Tukufu inawazungumzia watu wote kwa kuwa wana kitu ambacho wanashirikiana na kinawafanya wawe na nafasi ya kuwa karibu na kusaidiana katika mazuri na ya kumcha Mwenyezi Mungu, inasema kuwa watu wote pamoja na kutafautiana kwa dini zao, koo zao { Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi. Na tahadharini na Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwaangalieni. }(Anisaa:1)

Na Mwenyezi Mungu anawaambiwa kwa uwazi kabisa watu wote pamoja na utafauti walionao wa koo na tamaduni kuwa wana kitu ambacho kinawafanya wawe karibu na kuweza kuishi kwa pamoja na kwa amani, anasema { Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliyemchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari.}(Al hujuraat:13)

Sheria ya kiislamu inahifadhi utu wa mtu na heshima yake lakini pia katika makusudio yake yanaenea zaidi ya kuhifadhi nafsi, damu, mali, akili na heshima kwa ajili ya kulinda haki za maumbile, kwa ajili hiyo haki ya kuabudu kwa mtu kwa kutumia madhehebu yoyote na dini yoyote ni jukumu lake yeye mwenyewe mbele ya Mwenyezi Mungu, kwani dini hailazimishi mtu katika itikadi na kama ilivyokuja katika Qurani Tukufu {**Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.**} (Albaqara:256).

Kwa hivyo, ulinzi wa dini zilizoteremshwa na sehemu wanazoabudia ni miongoni mwa malengo ya kuujenga kuuimarisha uisilamu, Mwenyezi Mungu anasema { **Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki,ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu.Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba nyengine za ibada na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu.**} (Hajj:40)

Katika kuhitilafiana watu katika dini na kikoo kuna nafasi kubwa katika kuujega ulimwengu. Waislamu waliishi katika zama tofauti na tamaduni tofauti nazo tangu kushusha ujumbe wa mwanzo kabisa. Na historia ya kiutume imetupa mifano minne ya wazi kabisa ya kuweza kuishi pamoja na jamii tofauti, wa kwanza ni

kuishi na jamii iliyokuwa ikiwatendea uadui waislamu, waislamu walisimama kidete katika kujitetea ili wapate haki zao na uhuru wao wa kuabudu, kisha baada ya hayo, wakaendelea kuishi nao kwa kushirikiana kwa yale yote ya mazuri ndani ya jamii waliyotafautiana kiitikadi na mpaka wakahamia Habasha. Wakashirikiana na wahabeshi katika kujenga jamii yao na wakakubali kuwaona wengine wakiabudu kwa njia inayotafautiana na wao mpaka wakarudi tena mji wa Madina, wakawa wanatetea haki za watu wa dini tofauti katika kuabudu kile wanachokiamini na kukiitakidi. Na kuna katika mfano mingi na tofauti juu ya kukiri kwa Mtume (rehma na amani zimshukie). Katika mwaka wa wageni wa kinsara wa Najraan wa kumtembelea Mtume katika Msikiti wake Mtukufu. Na Msikiti ni nyumba tukufu ya waislamu. Na makanisa yao ambayo wanaabudu na kutekeleza ibada zao jambo ambalo waislamu halikuwakera, hivyo basi, kuyalinda na kuyahifadhi ikawa ni miongoni mwa haki kubwa sana za kuabudu.

Na kiongozi Omar Bin Al-Khatwab alifanya vizuri sana kwa kule kuzuia kutoondolewa nyumba ya Manasara (kanisa lao) katika Mji wa Mtakatifu, na kutaka lihifadhiwe na kutimiziwe ahadi yake, nayo ilikuwa ikijulikana kwa “upatanisho wa Kiomari”. Kwa ajili hiyo ikawa katika historia ya waislamu ni kawaida yao kulinda maeneo ya ibada ya wengine. Na tangu katika zama za mwanzo na mpaka alipokuja mwanazuoni wa kimisri Imam na mwanahadithi Allayth Bin Saad na imamu kadhi wa Misri Abdallah bin Luhay`a akasisitiza ya kuwa makanisa ya Misri hayakujengwa isipokuwa nyakati za uislamu, na kiongozi wa Misri kwa wakati huo alikuwa Harun Rashid, Mussa bin Isa akaamrisha kujengwa tena makanisa ambayo yalibomolewa na viongozi waliokuwa kabla yake na kuyafanya kuwa ni majengo katika mji, na walikuwa ni watambuzi wakubwa wa mji wao kwa wakati huo kuliko mtu mwengine yeyote. (angalia “Alwulatu walqadhau cha Kanady. Chapa Al aba Alyasuyuiin, Beirut mwaka, 1908H, Uk. 132.).

Kwa ajili hiyo, umuhimu wa kitabu hiki kilichotolewa na Wizara ya Wakfu ya Misri ambacho kinaweka wazi upande wa dini ya kiislamu ambao unaleta msamaha na utulivu kwa walio kinyume na itikadi hiyo. Hasa pamoja na watu walioteremshiwa vitabu ukaruhusu wafanye ibada zao katika maeneo yao ya ibada, na kuwawekea dhamana ya usalama wa maeneo yao ya ibada, ukaharamisha kuwatendea uadui kwa namna yoyote ile, na kwa namna hii ndivyo walivyokuwa waislamu waliotangulia katika historia na katika ustaarabu uliokuwa mzuri pamoja na maadili safi ambayo yalikuwa ndani ya nyoyo za watu kabla ya kuingia katika nchi za watu.

Profesa/ Shauky Alaam

Mufti wa Misri.

1. Ulinzi wa makanisa na athari zake katika kuuonyesha utukufu wa uisilamu

Ningelipenda kuanza maneno yangu katika sehemu hii kwa kuelezea mambo matatu yenye uhusiano na utafiti huu

Jambo la kwanza: dini itumiwapo katika sheria yoyote kwa malengo ya kisiasa basi matokea yake ni matatizo kwa watu na kwa mahusiano yao na kwa watu wenye sheria tafauti na wao. Na historia ni shahidi juu ya hili kwa nyakati zilizopita ambazo zilionyesha maafa makubwa kwa sababu ya makundi ya kidini kutaka kupata utawala wake kwa njia ya kisiasa.

Jambo la pili: Katika misingi madhubuti ya dini yetu ya kiisilamu, ni kuwa mwanaadamu yuko huru katika kuchagua itikadi aitakayo na kuamini kitabu kilichoteremshwa ambacho kina sheria na Mjumbe aliyeteremshiwa kitabu hicho. Ama malipo na hesabu za wote ni mbele ya Mwenyezi Mungu pekee asiye na mshirika, isipokuwa kwa muisilamu atalazimika kumuamini Mwenyezi Mungu na malaika wake na vitabu vyake vyote vilivyoteremshwa kwa Mitume bila ya kuwabagua kati yao. Na dalili ya haya ni, maneno yake Mwenyezi Mungu { **Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.** } (Albaqara:256).

Aya inajionyesha kuwa na nguvu za utendaji wa ibada, na kuwa ibada ndio yenye kuhukumu, ikiwa na maana ibada ndio inayopelekea maisha kuendelea na kuwepo kwa utulivu na usawa ambao hautakuwa na hofu wala wasiwasi na mfidhaiko na kulazimisha katika kuiamini fikira au dini.

Na katika sura Yunus, Mwenyezi Mungu anasema kumwambia Mtume wake (rehma na amani zimshukie) { Angelitaka Mola wako Mlezi wangelini amini wote

waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?}(Yunus:99).

Na aya inatosha kujieleza kuwa, utashi wa mtu umeshikamana na wa Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu, na ufahamu wa aya pia unaeleza kuwa haipasi kwa yeyote kumlazimisha mwengine kuingia katika dini yoyote kwani itakuwa ni kushindana na utashi wa Mungu ambaye utashi wake umepelekea kuwepo kwa tafauti kwa watu katika itikadi zao, anasema {Na Mola wako Mlezi angelipenda angewafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitalifiana,} (Hud:118). Kana kwamba kulazimisha ni utenganishaji wa imani na kuingilia utashi wa Mwenyezi Mungu.

Na mifano mikubwa mengine ya kuonesha misingi ya uislamu, ni kuwa, katika haki za watu ambao wanaishi chini ya kivuli chake na wakawa hawako katika dini hiyo ni kuwahifadhi juu ya itikadi zao na ibada zao mambo waliyoyarithi, na serikali nayo pia italazimika kuwalinda watu hawa.

Anasema Profesa Edmon Ribat katika maelezo yake kuhusu utukufu wa uislamu “ilikuwa ni haki kwa watu kunyenyekea nidhamu za utawala na kuhifadhi itikadi zake na tamaduni na waliyoyarithi, na hayo yalikuwa wakati ambao sheria iliyokuwa ikitawala ilikuwa ni ile ya kulazimisha watu wake kuingia katika dini za wafalme wao.”¹

Na ukweli huu umelezwa katika Qurani Tukufu na katika sunna za Mtume na Masahaba walikuwa wakitendea hali hii pamoja na waliowafuata.

Jambo la tatu: Qurani Tukufu imeeleza namna ya kutendeanana na watu wa vitabu kwa misingi ya wema na ucha Mungu, Mwenyezi Mungu anasema {**Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi**

¹ Gazeti la Sabah, toleo la 31, 1981.

Mungu huwapenda wafanyao uadilifu. 9. Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu.} (Mumtahirah:8-9).

Aya imewatenganisha wale walio katika dini tofauti katika makundi mawili: kundi moja lilikuwa ni la amani hawakuwa na mapigano na wala hawakuwatoa waislamu makwao, kundi hili lina haki ya kutendewa wema na urafiki, ni kama mfano wa wasio waislamu (wakiristo) wa Misri. Na kundi lengine lina uadui na uhasama na waislamu kwa kuwaua au kuwabugudhi ndani ya nchi au kujionesha kama kwamba wapo pamoja nao, kundi hili huwa ni haramu kushirikiana nalo kama mfano washirikina wa Makka. Aya ikiwa inamaanisha ya kuwa kundi moja katika haya halipaswi kufanywa kuwa ni marafiki na kuwatendea wema.

Hivyo basi, maadui wa taifa hawajaacha kutaka kuigawanya nchi “Misri” kwa kueneza sababu za mapigano baina ya makundi, kwa kupitia njia tofauti, na njia iliyo mbaya zaidi ni ile inayotumiwa ya kugawanya kati ya wananchi wa taifa moja ni njia ya udini kwa jina la uisilamu na ukiristo. Na adui anapofanikiwa kugawanya mshikamno huu uliokuwa kitu kimoja katika jamii ya kiarabu, basi athari yake na matokeo mabaya yake yataathiri kwa wote kila aliye muisilamu na asiye muisilamu (mkiristo).

Baada ya kueleza mambo matatu hayo, basi ifahamike kuwa dini haipaswi kuchukuliwa kama ndio njia ya kupitia katika kujiimarisha kisiasa, na pia ifahamike kuwa, miongoni mwa misingi madhubuti ya dini ni kutolazimishana katika dini. Na haki ya mwananchi ambaye anaishi ndani ya taifa ni kuhifadhi mambo ya dini yake na itikadi yake, na taifa (serikali) lina haki ya kuwahifadhi, kwani lengo la kuishi kwa pamoja kati ya waisilamu na wasio waislamu ni kitu kizuri kitakiwacho.

Na kwa kuwa tumekwishaelewa haya basi itakuwa ni wepesi kutaamali na suala zima la “ulinzi wa makanisa” kwa namna itakiwayo. Na kabla ya kusema dalili za kisheria kuhusu ulinzi wa makanisa kama ni jambo la lazima katika dini na kuyaharibu na kuacha kuyalinda ni kinyume na sheria, ningelipenda kusema haya: “Fatwa kubwa zitoleazo amabazo zinahusu masuala ya kitaifa na ya umma wa kiisilamu ambayo wanazuoni huyatolewa fatwa katika sehemu tafauti (huku na kule) zinahitajika kuwe na mlingano na mfanano wa fatwa hizo. Lakini iwapo fatwa hizo zitakuwa ni tafauti na zenye kukinzana hali hii itasababisha mchafuko na misukosuko ndani ya taifa.

Na tuonavyo katika matukio ya kuharibu nyumba za ibada kwa baadhi ya wasio na utambuzi, sababu yake inaweza kuwa ni:-

Sababu ya kwanza: kutokuwa na utambuzi (elimu ya sheria ya kiisilamu) au kutofahamu ipasavyo sheria zinazozungumzia kuhusu watu walioteremshiwa vitabu, hasa hasa makundi yenye misimamo mikali.

Sababu ya pili: kutokuwepo mwongozo (mitaala) ujulikanao kwa usahihi wa kuweza kufanya utafiti na uwekao wazi kati ya kazi za mufti na kazi za anayenukuu hukumu za kisheria kutoka katika mitaala hiyo. Na pia kutojulikana tafauti kati ya hukumu za kisheria zilizowafikiwa kwa pamoja kati ya wanazuoni na zile walizohitilafiana. Na kati ya hukumu zenye kulazimika kufikishwa na hukumu zenye mipaka ndani ya siasa teule. Vilevile kutokuwepo kwa wasomi (hasa) wa hadithi hukumu za watu walioteremshiwa vitabu.

Sababu ya tatu: kutojua kuchunga mazingira ya wakati, mahala, watu, mazingira na mambo yazukayo ya kielimu. Kwani hukumu za kisheria hutokea au kutotokea kwa kuwepo au kutokuwepo kwa kitu kilichosabababisha.

Sasa wacha nitoe dalili kuhusu masuala ya ulinzi wa makanisa, nikianza kwa dalili zifuatazo:-

Kwanza: Mwenyezi Mungu anasema { **Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba nyengine za ibada na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu.**} (Hajj:40)

Kitu ambacho kipo katika akili ya kila aliyesoma lugha ya kiarabu (nahau) ataelewa kuwa, Mwenyezi Mungu ametaja kuvunjwa kwa nyumba za watawa na makanisa na masinagogi na misikiti ameunganisha kuyataja majumba haya kwa “kiunganishi” cha “na”, na kiunganishi hiki kinajuulisha kuwa hukumu ya hayo yote ni moja kuanzia msikiti ambao husimamishwa ibada ndani yake na ambao kuuvunja ni haramu, hivyo inakuwa kuyavunja majumba mengine (yaliyotajwa ya ibada) huwa ni haramu vilevile.

Maana ya {**zingeli vunjwa (Mahekalu) nyumba za wat'awa,**} (Hajj:40) inakusudiwa, nyumba za watawa katika zama za Mtume (rehma na amani zimshukie) kwani zilikuwa zikimtaja Mwenyezi Mungu na sio zile zenye kuabudiwa masanamu.

Na ajabu yetu huzidi pale tusomapo kama alivyonukuu imamu Araazy kutoka kwa Kalby na Mukatil walipoifasiri aya {**na misikiti hutajwa sana ndani yake jina la Mwenyezi Mungu**} wakasema, hii inakusanya yote, wakimaanisha, nyumba za watawa, masinagogi, makanisa na misikiti, kwani Mwenyezi Mungu hutajwa ndani ya maeneo haya.²

Ama katika hadithi za Mtume (rehma na amani zimshukie) kwamba aliwasuluhisha watu wa Najiran na akawaandikia mkataba... “kwa jina la Mwenyezi Mungu... haya ni katika aliyoyaandika Muhammada Mtume na

² Atafsiri Ikabiir 40/23, 41.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu wa Najiran iwapo ana hukumu kwao.. kwa watu wa Najirani na majirani zao ni dhima ya Mwenyezi Mungu na dhima ya Mtume wake juu ya miji yao, mali zao, mila zao, kuuziana kwao, makasisi wao, maoskofu wao, waliopo miongoni mwao na wasiokuwepo miongoni mwao kuwa wasiwabadilisha oskofu katika maoskofu wao, wala kasisi katika makasisi wao, na wala wasichukuliwe kwenda kupigana jihadi na wala mali zao za zaka zisichukuliwe fungu la kumi”³.

Na katika zama za Sayidna Umar bin Al-Khatib kwa watu wa Ilyaa –Qudus- ameandika kupewa uhuru wao wa dini na kuharamisha kuyaharibu maeneo yao ya ibada na mambo yao:- “ haya ndio aliyoyatoa mja wa Mwenyezi Mungu Umar kiongozi wa waislamu kwa watu wa Ilyaa, kuwapa ulinzi na amani wa nafsi zao na mali zao na makanisa yao na sala zao na mila zao nyengine. Musikae katika makanisa yao wala musiyabomoe wala musipunguze kitu hata kama ni kidogo, hata msalaba wake, na chochote katika mali zao, wala musiwalazimishe juu ya dini yao na wala asidhuriwe yeyote katika hao, wala asijenge Myahudi yeyote katika Ilyaa.”⁴

Na sayidna Umar alipowaitikia wito wa watu wa Ilyaa akaingia Qudus na kuandika mkataba huu wa suluhu. Akaenda palipo na michanga na uchafu ukawa umezagaa juu ya jiwe akauondosha kwa nguo yake. Waislamu waliokuwa pembeni yake wakaanza kushindana katika kuondoa uchafu... kisha akaenda kulipo na uchafu uliozagaa kwa kuwekwa na mayahudi kwenye “Kanisa la Kiyama” akaanza kuondoa uchafu yeye mwenyewe, baada ya kuona hivyo waislamu nao wakaanza kushindana katika kuuondoa⁵.

³ Amuwal, Abi Ubaydah 1/244.

⁴ Taarikh Twabariy. 3/609 Chapa Maarif.

⁵ Bidaya wannihaya. 7/56

Na haya yalikuwa zama za sayidna Umar (Mwenyezi Mungu amwie radhi) na utendaji wake kwa mujibu wa sheria na hukumu za kiislamu zilizojaa uadilifu kati ya waislamu na watu walioteremshiwa vitabu, na watu walioteremshiwa vitabu wao wenyewe kwa wenyewe.

Kwa kuweka (kukunyua) daraja hili ni miongoni mwa malengo madhubuti ya sheria za kiislamu kwa maana hiyo sheria ikatilia mkazo jambo hili. Na miongoni mwa hayo ni kukubalika kutoa pongezi kwa muislamu kwa jirani yake na amjuaye na jamaa zake (wasio waislamu) kwa neema waliyoipata pasi na kuifanya dini kuwa ndio kitenganisho baina yao.

Na miongoni mwa hayo pia ni kukubalika kisheria mumpa mkono wa pole kwa nduguye asiye muislamu kwa kufikwa na msiba na kwenda kumtembelea awapo mgonjwa.

Na kitendo cha Mtume (rehma na amani zimshukie) kumtembelea kijana wa kiyahudi, hadithi hii inajulikana na ni maarufu.

Kuunganika huku kwa kuishi kwa pamoja na watu wa dini zilizoteremshiwa vitabu hii inatokana na kuamrisha kwenu na sheria ya Mwenyezi Mungu.

Pili: Miongoni mwa misingi ya kiislamu ni “kuondosha (kuzuia) matatizo” ni mafunzo yaliyochukuliwa ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu ambayo yanahimiza umuhimu wa kuwa pamoja kwa kuwa katika amani kwa masilahi ya mwanaadamu kupitia sheria na kitabia. Na kuwepo kwake ni kuzuia matendo mabaya na isifikie kuwa kila mwenye haki achukue haki yake hata kama ni kwa kumdhuru mwengine. Nao msingi huo ni chanzo cha sheria na maadili yaliyo sawa yenye kutambulikana katika sheria za wanaadamu pia, (sheria za kuwekwa).

Na chimbuko la sheria hii tukufu ni Qurani Tukufu kama aya nyingi zinavyoelezea, kwa mfano; { Wala msiwatukane hao wanao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua } (Al anaam:108).

Kuyaharibu makanisa na kuondoa mambo yao wanayoyatakasa ni sababu ya watu wa dini ya kikiristo nao kuiharibu misikiti ya waislamu. Na kila chenye kupelekea hayo basi ni lazima kizuiliwe.

Tatu: Masahaba (radhi za Mwenyezi Mungu ziwashukie) walifungua miji mingi na wala hawakuvunja makanisa, kwa ajili hiyo, kukiri kwao Masahaba na wanazuoni na watambuzi waliokuja baada yao ni dalili tosha ya kuwa si halali kuyavunja na kuyabomoa.

Nne: ajibu wa kiongozi aamrishe kulindwa makanisa na kutofanyia vitendo vya ukiukwaji kwa kwenda sambamba na utambuzi wa kisheria wa siasa ambao unasimamia pia kulinda malengo ya sheria na masilahi ya viumbe na kuweza kutumika sawa masilahi yaliyopo na kujiepusha na matatizo yaliyopo pindi masilahi na matatizo yatakuwa yamekutanika katika sehemu moja.

Tano: Wasomi na wanazuoni wametamka neno (tamko) lao la pamoja tangu mwanzoni mwa ufunguzi wa kiisilamu kwa kukiri kuwa miji waliyoifungua wameifungua kwa amani. Imam Ibn Qudama anasema: “neno la pamoja limepatikana juu ya suala hilo na lipo pasi na kuwepo wa kupinga.”⁶

Neno “Suluhisho” linakusudiwa yale yote yaliyokuwa yakitokea kati ya waislamu na wasio waisilamu kupitia mikataba na makubalino na yale yanayojiri hivi sasa katika jamii ya wanaadamu kutokana na mikataba, katiba na makubaliano, haya yote ni makubaliano na inalazimu kuyatimiza.

Na kutokana na dalili zilizotangulia za ndani ya Qurani Tukufu na za ufahamu na za kiakili, itafahamika wazi kuwa uisilamu umeweka uhuru kwa mtu kuwa na itikadi aitakayo, na kutofaa kumlazimisha katika kuingia katika itikadi nyengine, na inalazimika pia kuwalinda watu wa dini zilizoteremshiwa vitabu waishio katika miji ya waislamu, na pia kutofaa kuwaingilia katika mambo yao ya kiibada.

⁶ Almughniy, 9/284

Sayidna Umar (Mwenyezi Mungu amwire radhi) anasema katika mkataba wake kuwaambia: “nyinyi muko salama kwa damu zenu, mali zenu na makanisa yenu hayatakaliwa na wala hayatabomolewa.” Je, kuna ushahidi mzuri kuzidi huu? Na katika kitabu cha Ibn Shuiyba kuwa Umar (Mwenyezi Mungu amwie radhi) amewaandikia wafanyakazi wake kuwa wasibomowe nyumba ya watawa, wala kanisa, wala nyumba ya wanaoabudu moto.”⁷

Hivyo umekwishaona dalili nyingi ambazo zinasisitiza kuwa haipasi kuharibu maeneo ya ibada kwa mfano makanisa na maeneo mengine. Si hivyo tu bali Qurani Tukufu na mikataba ya amani aliyoweka Mtume (rehma na amani zimshukie) na masahaba zake na waliowafuata kwa watu walioteremshiwa vitabu haya yote yanajulisha kuwa uisilamu unawahifadhi watu wa vitabu na itikadi zao na mambo yao ya kiibada na makanisa yao. Na historia ya kiisilamu kwa miaka mingi ina dalili tosha ya kuthibitisha jambo hili. Na upole wa uisilamu na kujengeka kwa ustaarabu wake kwa kutaamali na watu wa dini tofauti, na hasa watu wa dini zilizoteremshiwa vitabu.

⁷ Musnaf Ibn Aby Shaybah. 6/467.

Ulinzi wa makanisa katika uisilamu⁸

Ulinzi wa makanisa ni kitu kitakiwacho katika uisilamu na chenye kuambatana na misingi madhuti ya kiisilamu, nayo:-

Kwanza: Kuhifadhi dini, dini ni mkusanyiko wa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu kwa njia ya wahyi juu ya wajumbe wake kuanzia Adam mpaka Mtume wa mwisho Muhammad (rehma na amani zimshukie), mkusanyiko wa hayo yote ndio dini.

Na kila alichokuja nacho Nabii miongoni mwa Manabii, na kutumwa kwa watu wake zikiwemo sheria, mfano, sheria ya Mtume Ibrahi, Mtume Mussa, Mtume Issa na Mtume Muhammad rehma na amani ziwashukie wote.

Na ilivyokuwa sheria zote zilizoteremshwa kwa Manabii zinawafikiana katika misingi yake, nayo ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake, na vitabu vyake, na Mitume wake na siku ya mwisho, na kama zinavyokubaliana na uhifadhi wa masilahi ya mwanaadamu ambayo kwa ajili hiyo ndio Mwenyezi Mungu akaiteremsha dini yake kwa Mitume wake –rehma na amani ziwashukie- na masilahi hayo ni kuhifadhi kwa dini, nafsi, akili, heshima na mali, kwa kuwa masilahi haya ni miongoni mwa mambo ya lazima katika maisha ya zama zozote, na wala hayatofautiani katika njia ya kuyahifadhi kutoka katika sheria hadi sheria nyengine.

Kwa ajili hiyo ikawa ni kitu cha makubaliano kwa sheria zote, kama zilivyowafikiana sheria hizo katika kuhifadhi maadili ya kiutu na tabia njema kwa mfano kutimiza ahadi, ukarimu, ukweli, uaminifu na tabia nyengine nzuri na kuharamisha kinyume na hizi kwa mfano, kutotimiza ahadi, ubahili, khiyana na tabia nyengine ovu. Kwa ajili hiyo sheria ikawa na kitu kinachounganisha maadili

⁸ Utafiti huu umeandikwa na Profesa Abdallah Najjar, mkuu aliyetangulia wa Kitivo cha masomo ya juu ya chuo Kikuu cha Al azhar na ni mwanachama wa utafiti wa kiisilamu.

haya ya kidini na kufanya kuwa ni kitu chenye kulazimika kulindwa (kuhifadhiwa) na kukemea pindi kitaachwa kulindwa.

Iwapo mambo haya ni katika mambo muhimu ya kidini, na ni misingi ya kiutu ambayo ipo katika sheria zote zilizoteremshwa na ni nguzo madhubuti miongoni mwa nguzo za dini, basi kuhifadhi dini pia itajumuisha kuhifadhi na maadili haya yliyopo katika sheria zote zilizoteremshwa na pia itakusanya kuhifadhi maeneo ya ibada.

Pili: Utajo wa Mwenyezi Mungu unahitajika kwa waisilamu na kwa wasio waisilamu, na hata kama haamini dini yoyote, tafsiri ya aya **hii {Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa nymba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi.}** Alhaji:40. Anasema Kurtubiy “ Mwenyezi Mungu ametaja maeneo ya ibada ya watu wa dini zilizotangulia, nazo ni maeneo ya watawa, masinagogi na misikiti ya waisilamu; kwa sababu watu wa majengo haya ni wale walioteremshiwa vitabu hapo kabla na ndani yake kuna mambo ya lazima ya kuhifadhiwa.”⁹ . kwa ajili hiyo, maeneo ya ibada ni lazima kulindwa na kuyahifadhi na wala haipasi kuyabomoa.

Na kama ilivyokuwa utajo wa Mwenyezi Mungu ni kitu kitakiwacho kwa kila mtu basi kile ambacho kitamsaidia mtu katika kufanikisha utajo huo basi huwa ni jambo litakiwalo, na kila likufikishalo katika kile ukitakacho basi huwa ni kinatakikana kiwepo.

Tatu: Mwenyezi Mungu ameharamisha kulazimisha watu katika kuamini baada ya kusema kuwa imani ni miongoni mwa uhuru na ukinaifu wa mtu. Amesema **{Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu}**(Albaqah:256). Na kutokana na utashi wa Mwenyezi Mungu wa

⁹ Kurtubiy, Jaami` Ahkaam Alkuraan. 2/72.

kuwapa waja wake uhuru wa kuchagua kuamini hii haina maana kuwa tuwatendee kinyume na haki ya uchaguzi wao. Kwa mfano kuwaadhibu kwa kuwatuma wengine waende na kubomowa majengo yao ya ibada, na kama watajitokeza kufanya hivyo basi itakuwa ni kwenda kinyume na kukengeuka yale aliyokiri Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Na katika mambo yasiyo na shaka ndani yake kubomoa (kuharibu) maeneo ya ibada ya wasio waisilamu na kushawishi wengine kufanya hivyo ni sawa na kumpinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake na itapelekea kuonekana kuwa kuna ulazimishaji wa kidini na upungufu wa malengo ya uwepo wa dini ya Mwenyezi Mungu kwa viumbe vyake.. na Mwenyezi Mungu alipompa hiyari mwanaadamu kuchagua imani na kulazimika kuyatenda yale yaliyomo kaika imani hiyo, basi kumlazimisha katika dini huwa ni haifai (haramu). **{Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu}** maneno haya matukufu yanamaanisha makatazo, ikiwa na maana musimlazimisha yeyote kuingia katika dini ya Mwenyezi Mungu, na afanyaye hayo ya kulazimisha kwa namna yoyote kwa mfano kubomowa makanisa atakuwa amefanya kitu kilichokatazwa katika dini na kilichoharamisha kisheria, haifai kutenda haya.

Nne: Haki ya wasiokuwa waisilamu katika kuhifadhi makanisa yao itategemea utekelezaji wa waisilamu wa ahadi zao, wasomi wa zamani wameelezea ufahamu huu kwa zile nchi ambazo zimefunguliwa kwa kuwepo kwa suluhisho, au kwa kuwafikiana kwa watu wake, mfano nchi ya Misri ambayo ilionyesha ushirikiano wake wakati wa ufunguzi wa kiisilamu. Maeneo ya ibada yalikuwepo katika nchi hiyo na wala haipasi kuyagusa kwa kuwa ni lazima halindwe, na ni haki kwa watu wake kuyafanyia marekebisho yale yaliyoharibika.¹⁰

¹⁰ Ibn Qayim – Ahkaam Ahlu Dhima 121-130.

Suluhu ambayo wasomi wa fiqhi (watambuzi) wameielezea, imekuwa ni msingi mkuu wa kuharamisha maeneo ya ibada kutofikwa na matatizo na hali hii ikaendelea hadi wakati wetu wa sasa na kuwekwa hata katika misingi ya kikatiba ambayo inakiri usawa kati ya watu wa taifa moja. Na kuharamisha ubaguzi kati yao kwa sababu za kidini au sababu nyengine yoyote kama utaifa, rangi, lugha, na nyenginezo ambazo husababisha ubaguzi katika jamii ya kiislamu. Na kuharamishwa huko kunahitajika kuwe ni kwa misingi madhubuti ya utaifa ili wananchi wa taifa moja waweze kusaidiana katika mema na mazuri na si katika mabaya na maovu.

Na iwapo misingi ya kikatiba imeweka usawa kati ya wanataifa moja bila ya kuangalia tafauti zijitokezazo, basi makubaliano hayo ni lazima yatekelezwe kwa kuyafanyia kazi maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema {**Enyi mlio amini! Timizeni ahadi.**} (Almaida:1). Haipasi kuvunja makanisa au kuyateka.

Tano:

Siasa ya kujenga makanisa ipo kama rehani katika jamii, na kiongozi ndiye mwenye jukumu la kupima masilahi hayo na kukadiria kwa mujibu wa aonavyo na kwa kuchunga hisia za udini, pindi akiona idadi kubwa ya wasio waislamu imezidi na inahitajika kujenga makanisa basi hana budi kuitikia wito huo, na aonapo kuwa hakuna haja ya kufanya hivyo basi atachunga masilahi ya umma pasi na kuathiri itikadi ya dini ya mwengine. Mtume (rehma na amani zimshukie na Masahaba wamewaachia wasio waislamu kila walichokuwa wakikihitaji katika kanisa 11.

Anasema Ibn Qayim: “ kufupisha maneno ni kusema, iwapo idadi kufupisha maneno ni kusema, imamu atawafanyia waislamu kilicho na masilahi zaidi kwa mujibu wa wingi au uchache wa wasio waislamu, iwapo idadi yao ni ndogo

¹¹ Ibn Qayim – Ahkaam Ahlu Dhima.

atawabakishia idadi inayowatosheleza ya makanisa, na iwapo idadi yao ni kubwa itabidi azibe pengo hilo ya uwepo wa makanisa ambayo wanayahitaji.¹²

Sita: dalili za kisheria zimepo nyingi za kuwa haipasi kuvunja makanisa, nazo ni kama zilivyotajwa katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume (rehma na amani zimshukie) na mienendo ya Masahaba zake.

Ama zilizomo katika Qurani Tukufu:

1. Mwenyezi Mungu anasema **{Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa nyumba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi.}** (Hajj:40)

Na dalili katika aya hii ni: Mwenyezi Mungu Mtukufu Ameeleza kwa waja wake namna ya kujikinga na kufanya uadui katika maeneo ya ibada ya dini zote zilizoteremshiwa vitabu, na lau kama watu hawajajikinga na uadui huo basi pasingelibakia kitu na kutoweka athari zake zote.¹³ Na imekuja aya kama ni amri ikamaanisha kuwa kuepusha matatizo katika nyumba za ibada ni kitu kitakiwacho na uharibifu huwa hautakikani.

2. Hadithi za Mtume (rehma na amani zimshukie)

Impokewa kutoka kwa Ar-wa bin Zubeir (radhi za Mwenyezi Mungu ziwashukie) amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani zimshukie) amewaandikia watu wa Yemen kuwa, yeyote awaye kama ni Myahudi au Mnasara basi asifanyiwe fitina.¹⁴

¹² Ibn Qayim – Ahkaam Ahlu Dhima. Uk 131.

¹³ Qurtubiy. Uk 70 (kitabu kilichotajwa hapo juu)

¹⁴ Abu Ubayd – Al amuwaal. Uk 35.

Dalili ya hadithi ni kuwa, Mtume (rehma na amani zimshukie) amekataza kufanya fitina kwa asiyekuwa muisilamu, na fitina ni kule kufanya ushawishi juu ya imani anayoitakidi, ikiwemo kuvunja makanisa, kwa maana hiyo uvunjaji wa makanisa kwa mujibu wa hadithi hii makatazo.

3. Mienendo ya Masahaba

Iliyopokewa na Umar bin Al-Khatib (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) ni kuwa amesuluhisha watu wa Humus kuwa wapate usalama wa nafsi zao, mali zao na nyua zilizozunguka mji wao na makanisa yao na ikaandikwa katika mkataba ambao amewapa watu wa Qudus: yeye amewapa usalama wa nafsi zao, mali zao makanisa yao na misalaba yao, kuwa katika makanisa yao asikae mtu yeyote na wala yasibomolewe, na wala yasipunguzwe kitu hata kama ni kidogo hata msalaba wao na chochote katika mali zao na wala wasilazimishwe kuhusu dini yao na wala asidhuriwe yeyote.”¹⁵

Na ikaja katika mkataba ambao Amru bin Aas (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) kwa watu wa Misri, imeandikwa: “ Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu, haya ndiyo aliyowapa Amru bin Aas watu wa Misri kuhusu usalama wa nafsi zao, mali zao mila zao, makanisa yao, bara lao na bahari yao na kuwa wasipunguziwe chochote katika hayo. Na mkataba huu ni dhima kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kiongozi wa waumini na kwa waisilamu.”¹⁶

Saba: Ama kuhusu dalili zilizopokewa ambazo zinakinzana na dalili hizi basi ifahamike kuwa ni dalili zenye kuelezwa katika matukio ya kisilaha ambayo pande mbili huwa tayari zimeshakamilisha kila aina ya utaratibu wa kupambana na hakuna tena muda wa kuepukana na tukio hilo, na ikawa ilaka kati ya

¹⁵ Al baladhiy – futuuh Buldaan – Uk 131. Al kharaaj Abiy yussuf – uk 148...

¹⁶ Anujuumu Zaahirah. 1/Uk 24.

waisilamu na wasio waisilamu ipo katika mahakama za mikataba ya kimataifa ya suluhisho ambayo huzuia kufanya uadui kwa upande mwingine. Na mikataba yenye kuhakikisha kila mtu anapata haki ya kuishi kwa usawa na mwingine ndani ya nchi au nje. Ukiachilia mbali ilaka iliyopo kati ya waisilamu na wakiristo ndani ya Misri tangu zamani na kuenea kwake kwa amani na usalama pamoja na ushirikiano wa kuijenga nchi kwa pamoja.

Ieleweke kuwa hukumu za kujitahidi hubadilika kwa kubadilika nyakati zake na mahala mwake na mazingira yake, hivyo pengine haziwezi kuwa ni hoja kwa baadhi ya nyakati, ama kuhifadhi makanisa ni jambo ambalo hakuna tofauti na fatwa zitolewazo na wafuasi wa kundi la wapiganaji wa Dola la Kiisilamu ((IS) ni fatwa ambazo zinazichezea shere kitabu cha Mwenyezi Mungu na hukumu za dini yake kwa ajili ya kujifurahisha nafsi zao mbaya. Hizo ni fikira potofu hazina ukweli wowote wa dini na wala hakuna hukumu inayoambatana na wanayoyasema, kwa ajili hiyo haifai kuwategemea kwa yale wanayoyasema na wanayoyaitakidi ya kuwa na wajibu wa kuyavunja makanisa kwa sababu wayasemayo hayapo na wala hayajasihi na yanapingana na misingi na malengo ya dini sahihi. Hivyo, kwa waisilamu ni lazima wayalinde makanisa kwani sheria na dalili zake inaruhusu jambo hili.

Ulinzi wa makanisa katika uisilamu¹⁷

Upole wa uisilamu umefikia kiwango cha kuwatendea walioteremshiwa sheria tafauti zilizotafautiana nazo katika ibada na itikadi, upole ambao umewaacha wawe wakiabudu kila watakacho, na kuwapa uhuru wa kuchagua itikadi ambayo wanaona ni mnasaba kwao. Haukumlazimisha mtu kuacha dini yake, na wala kumkazania kuacha itikadi yake. Kwa maana hii Mwenyezi Mungu anasema **{Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anaye mkataa Shet'ani na akamuamini Mwenyezi Mungu bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.}** Albaqara:256.

Na kauli hii ndio waitumiayo wasomi na maulamaa. Anasema Ibn Kathiir katika tafsiri yake “ina maana kuwa, musimlazimisha yeyote kuingia katika dini ya kiisilamu, kwani dalili zake na uongofu wake uko wazi kabisa na wala hauhitaji mtu kulazimishwa. Lakini kwa atakayemuongoa Mwenyezi Mungu na kuuwepesisha moyo wake na kuweka mwanga ndani yake na akaingia katika uisilamu basi hakuna tatizo.”¹⁸

Uisilamu umehalalisha kwa wasiokuwa waisilamu kufanya mambo yao ya kidini pasina kubomolewa Majengo na Makanisa yao wala kuvunjwa Misalaba yao. Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya watu wa dini tofauti isemayo “wana wao (katika manufaa) kile ambacho nasi tunacho na pia wana wao (katika hasara) kile ambacho tunacho” na “ tunawaacha na kile wanachokiabudu.” Hizi ni

¹⁷ Utafiti huu ameuandaa Prof; Muhammad Abdul Sataar Aljibaal. Mhadhiri wa kitivo cha sheria na kanuni – Chuo Kikuu Cha Al azahar.

¹⁸ Tafsiri Ibn Kathiir. 1/310. maktaba Aturaath Al islamiy.

kanuni ambazo hutamkwa na wasomi na maulamaa na kuna matukio ambayo yanatilia mkazo jambo hili.

1. Barua ya Sayidna Umar bin Abdul Aziz (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie): “ msivunje nyumba za watawa wala kanisa wala nyumba za wanaoabudu moto.”¹⁹
2. imepokewa na Ataa kuwa aliulizwa kuhusu kanisa je hubomolewa? Akasema: “Hapana”.²⁰

Kwa ajili hiyo, kutokana na misingi ya kiuzalendo ambayo inakusanya baina ya waisilamu na wasio waisilamu ndani ya taifa, watu wenye dini nyengine za kiyahudi, kinasara wana haki ya kufanya ibada zao za kidini ndani ya majengo na makanisa yao, bila ya kuhisi hofu katika nafsi zao na majengo yao. Na wana haki ya kufanya marekebisho ndani ya kanisa pale atakapotoa ruhusa kiongozi kwa kigezo kile kile kilichofanyika katika miji ambayo waisilamu waliifungua kwa amani. Kwa ajili hiyo, wasomi na maulamaa wameruhusu kufanya mabadiliko yanayohitajika ndani ya makanisa pale kiongozi atakapotoa amri, kwa mujibu wa utambuzi (fiqhi) wa kisheria za kisiasa ambayo inachunga pia masilahi ya sheria na masilahi ya viumbe.

Na iwapo asili ni kuwaacha na kile wanachokiabudu, hivyo basi, wao watakuwa wana kawaida kama ya kupiga kengele kwa mujibu wa itikadi yao ndani ya makanisa yao na kusoma Injili na taurati ndani yake, na katika yenye kujulikna haya yote hayafanyiki isipokuwa ndani ya majengo ya ibada, hivyo, haitopasa kuyabomoa (kuyavunja) majengo haya.²¹

¹⁹ Imepokewa na Ibn Abi Shaybah – kitabu cha jihadi – dar Fikri

²⁰ Imetolewa na ibn Abi Shaybah –kitabu cha jihadi.

²¹ Al badai`u Wasanai`u Lil kasaniy 5/4336.

Na iwapo maulamaa wanaona kuwa watu hawa hawazuiliwi kufanya mambo ya ibada zao ambayo wanaona ni sawa, hivyo haitosihi kusema kuwa inafaa kubomolewa majengo ya ibada zao, hii ikiwa na maana kutokana na uongofu wa uisilamu unakataza kabisa kabisa kuvunja nyumba za ibada sawa nyumba za watawa, makanisa. Nao ni uongofu wa Mtume (rehma na amani zimshukie) alipousia wasia mwema wa mwisho wa masiku yake kwa watu wanaoishi katika ardhi ya waisilamu kwa mikataba (dhima) aliposema: “Ninamuusia atakayeshika uongozi baada yangu mimi kuhusu watu wa dhima (wasio waisilamu) kutendewa wema. Na kuwapiga vita wale anaowapinga, na wala wasilazimishwe kwa kile wasichokiweza.” Na kama ilivyokuwa katika masiku yake alikuwa akiwausia wafanya kazi wake kuwatendea wema watu wa dhima, na kuwataka kuchanganyika nao ili wahisi kuwa nao wanatendewa muamala mzuri.²²

Na katika vitu ambavyo hatuhitaji kuvisahau ni muamala wa waisilamu kwa watu wa miji waliyoifungua ambao ulikuwa na uadilifu na usawa na kutowafanyia uadui, mfano mzuri zaidi ni wa saydna Amru bin Aas (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) pamoja na wa Kibti wa Kimisri, alipowaondoshea makero na usumbufu mpaka wakapata upendo kutoka kwao na wakamtii kwa amani na kuupenda utawala wake.

Na ukweli ni kuwa, waisilamu walikuwa wanawajali sana wakiristo wa kimisri, kwani Mtume (rehma na amani zimshukie) amewausia kheri, akasema: “ mtakapoifungua Misri wausieni Wakibti kheri kwani wao wana dhima na uhusiano wa unasaba .”²³

²² Tarekhe rusul walmuluuk – Atabariy. 2/449.

²³ Ameitoa hakim – Almustadrik. 2/553. hadithi ni sahihi kwa masharti ya Bukharin na Muslim.

Na kwa nini isiwe hivyo wakati waliweza kuweka sheria na kanuni ndani ya nchi ambayo wanaishi kwa pamoja kati ya waisilamu na wasiokuwa waisilamu ndani ya chombo kimoja ambacho kimeweka sawa haki kwa wote.

Na iwapo huu ndio msimamo wa Mtume (rehma na amani zimshukie) kwa wasio waisilamu basi iweje tusome maneno ya wanaopinga umoja wa umma na kuamrisha kuvunjwa na kubomolewa kwa makanisa au kusababisha maafa, wakati ambao hawajatosheka kwa waliyoyasema maulamaa na wasomi wa kiisilamu wa kuwausia mema watu wa dini zilizoteremshiwa vitabu. Kwa ajili hiyo imam Abu Yusuf amemuandikia kiongozi harun Rashid akimuusia kuhusu watu wake na kuwaangalia hali zao ili wasidhulumiwe na wala wasiudhiwe na wala wasilazimishwe kitu kilicho nje ya uwezo wao. Na kama kiongozi wa kiisilamu atatoa agizo ambalo litawakera wasio waisilamu basi wasomi na maulamaa huwa wanachukia jambo hilo.

Na kutokana na hayo yaliyotangulia, basi inakuaje kuvunjwa kwa makanisa? Na kwa upande wa taifa ni lazima walinde ulinzi ambao hautokusanya uadui wa ndani tu pekee bali pia na uadui utokao nje. Imam Laythiy (Mwenyezi Mungu amrehemu) ametoa fatwa wakati mmoja wapo ametekwa ngawira “nionavyo wampeleke katika nyumba ya mali na wamuandikishe kama ni mtu wa dhima.” Na iweje yavunjwe makanisa yao na uisilamu umekiri uhuru wa kuabudu, na umeamrisha kuwa halazimishwi mtu kuingia katika uisilamu. Ingawa unalingania watu wote lakini ulinganiaji ni kitu na kulazimishani kitu chengine kabisa. Kulingania kumesharutishwa, ama kulazimisha ni kumnyima mtu uwezo wa kuwa na hiari na kumekatazwa. Mwenyezi Mungu anasema { **Hapana kulazimisha katika Dini.** } **Albaqarah 256.** uhuru wa itikadi katika uisilamu ni haki yenye dhamana.

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani zimshukie) anawakumbusha Masahaba zake moja ya alama za utume wake kwa kusema, “nyinyi

mutaifungua Misri, nayo ni ardhi inayoitwa Qerati basi wausieni watu wake mema, kwani wao wana dhima na uhusiano wa unasaba .” Mtume (rehma na amani zimshukie) anawausia watu wa Misri mema pamoja na kuwa wakati huo walikuwa ni Maqibti (si waisilamu).

Huo ndio wasio wa waisilamu kwa wasiokuwa waisilamu, wasia wenye kuonyesha –bila ya shaka – upeo mkubwa kiasi gani juu ya rehema na upendo wa dini ya kiisilamu katika muamala wake.

Na Umaru ibin Aas alitekeleza msamaha huu kivitendo alipofungua Misri, kwani alitoa uhuru wa dini kwa Waqibti na kurejesha Batrayark Benyameen uongozi wa kiqibtiya katika kiti chake baada ya kutoweka karibu miaka kumi na tatu. Si hivyo tu bali aliamrisha kupokelewa kwa sherehe alipotemtembelea mji wa Al-askandareah. Huu na mifano mengine inaonesha ukubwa wa upendo kwa wasio waisilamu, wa kuwapa uhuru wa kidini ambao inabidi kuwaruhusu kufanya ibada zao na mambo yao ya kidini ambayo inapaswa kutovunjwa makanisa yao au kuyafanyia aina yoyote ile ya uadui.

Huu ndio msimamo wa kiisilamu na yapaswayo kutolewa katika fatwa za kisasa katika maudhui hii.

Ulinzi wa makanisa katika uisilamu²⁴

Kwa kuanzia na makusudio ya sheria na lengo la Qurani Tukufu kwa ujumla kuhusu upole na usamhevu na rehma na wepesi na kusaidiana katika mema na ya ucha Mungu tunasema, Mwenyezi Mungu atuwafikishe.

Uvunjaji wa makanisa au vitendo vya uadui katika makanisa kwa namna yoyote ile ni harmu kisheria, kwa dalili zifuatazo:-

Kwanza: haikuja katika Qurani Tukufu au katika hadithi za Mtume (rehma na amani zimshukie) kuwa zimeamrisha jambo hili, isipokuwa zimekuja amri za kuyafanyia matengenezo na kuyahifadhi. Na kuhifadhi haki za watu wa dini nyengine zilizoteremshiwa vitabu. Nayo ni mojawapo ya malengo ya sheria tukufu yenye kuhimiza kulinda na kuihifadhi, Mwenyezi Mungu anasema {**Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa nymba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi.**} (Hajj:40). Ikakatazwa kuvunja makanisa na mfano wake kwa kuwa ndani yake munatajwa jina la Mwenyezi Mungu kama walivyokuwa watu wenyewe kwa wenyewe wanasaidiana katika kuihifadhi ardhi (nchi) kuepukana na uharibifu.

Pili: namna alivyotaamali Mtume (rehma na amani zimshukie) na watu walioteremshiwa vitabu wa Madina na katika visiwa vya Uarabuni na Yemen, haikupokewa kutoka kwake kwamba aliamrisha kubomolewa kitu chochote au kufanya tendo la uadui, lakini kilichothibiti kutoka kwake (rehma na amani zimshukie) ni kuwa aliwakataza waisilamu waliofungua miji kuacha kubomoa au kuua watawa na wanawake na watoto katika vita.

²⁴ Utafiti huu umeandaliwa na Prof; Muhammad Nabil Ghanayim. Mhadhiri wa sheria ya kiisilamu. Kivito cha dar Uluum – Chuo kikuu Cha Kairo.

Tatu: Masahaba wa Mtume walipita njia ile ile aliyokuwa akiipita Mtume (rehma na amani zimshukie), haikupokewa kutoka kwao kuwa kuna yeyote miongoni mwao alivunja kanisa au aliamrisha kulifanyia uadui, lakini walikuwa wakihifadhi na kukubali kuwepo, kama alivyofanya sahaba Umar bin Al-Khatib (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) wakati wa kufungua nyumba tukufu ya Qudsi aliposali nje ya kanisa ili asije akatokea yeyote na kuweza kulifanyia vitendo vya kiuharibifu au kuligeza na kulifanya kuwa ni msikiti; kwani alisali nje kwa lengo la kulihifadhi, si hivyo tu, bali aliandika mkataba wa kulindwa na haki nyenginezo.

Nne: Viongozi waliofungua miji waliotumwa na Mtume (rehma na amani zimshukie) pamoja na Makhalifa walioongoka, walisimama kidete kulinda makanisa hayo nchini Misri, Sham, Iraq na miji mengine haikupokewa kutoka kwa Saad bin Aas nchini Iraq wala kwa Khalid bin Waliyd nchini Urduni, wala kutoka kwa Ubaydah bin Jarah kutoka Sham wala kwa Amru bin Aas kutoka Misri wala haijapokelewa kutoka kwa yeyote katika miji mengine ambayo ilikuwa na makanisa kuwa ameamrisha yabomolewe au kufanyiwa vitendo vya kiuadui, lakini imethibiti kinyume nayo ni kuyalinda na kuyahifadhi.

Na historia imekuwa ndio shahidi wa haya tangu karne kumi na tano hatukusikia wala kusoma kuvunjwa au kushambuliwa kwa makanisa na majengo mengine ya ibada isipokuwa kwa watu madhalimu ambao kazi yao ni uharibifu wa kila kitu ndani ya miji ya waisilamu kiuadui na kiuhasama kama ilivyotokea katika vita ya Matatari. Ama waisilamu sawa wawe viongozi au raia wa kawaida hawakufanya jambo hili.

Tano: Uisilamu umeamrisha kwa amri za wazi kabisa kuwa watu wa vitabu watendewe muamala mzuri na ukakiri kuwa wana haki sawa na sisi, na mwenye kuwafanyia makero basi Mwenyezi Mungu na Mtume wake wako mbali na uovu huo kwani atakuwa amemkera Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hivyo

inalazimika kuwatendea wema, uadilifu na usawa, Mwenyezi Mungu anasema { **Basi wakikujia, wahukumu baina yao au jipuuze nao. Na ukijipuuza nao, basi wao hawatakudhuru kitu. Na ukiwahukumu, basi hukumu baina yao kwa uadilifu. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda waadilifu.} Al maida:42.**

Na mifano mengine ni: Muisilamu kumuoa mwanamke wa watu walioteremshiwa vitabu na kumwezesha kufanya ibada zake katika kanisa kwa mujibu wa sheria zake. Pia kula chakula chao kama ilivyosemwa katika Qurani Tukufu { **Na chakula cha walio pewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao. Na pia wanawake wema miongoni mwa Waumini, na wanawake wema miongoni mwa walio pewa Kitabu kabla yenu, mtakapo wapa mahari yao, mkafunganao ndoa, bila ya kufanya uzinzi, wala kuwaweka kinyumba.} Al maida : 5 Na sheria nyengine zisizokuwa hizi.**

Sita: Watu wa makanisa haya ni sehemu katika raia wa nchi moja ambao umoja wao umethibiti na tamaduni zao ni moja na hisia pia. Na wakasaidiana kati yao mpaka wakawakama ni familia moja, sasa iweje tuwagawanye na kuwatenga katika haki iliyothibiti katika kila mmoja wetu?

Tuhifadhi haki ya taifa sawa kwa muisilamu na asiyekuwa muisilamu mpaka tuwe ni mkono mmoja juu ya adui wa taifa walio nje ya sheria, tuishi kwa pamoja katika amani na usalama “ wana haki kama zile tulizonazo.”

Saba: kanuni ya kisheria inaeleza kuwa, haifai kufanya uadui isipokuwa kwa maadui wanaotushambulia kwa kuwarudishia uadui wao. Mwenyezi Mungu anasema { **Anaye kushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadiri alivyo kushambulieni. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wachamngu.} Albaqar:194.**

Na hakuna hata mmoja katika ndugu zetu wa kikiristo walioifanyia uadui misikiti yetu lakini walisimama katika kuitetea na kuihifadhi na kusaidia katika ujenzi wake. Basi iweje waislamu wanayafanyia uadui makanisa yao na wala

hawayahifadhi kama (wakiristo) wanavyohifadhi misikiti yetu, kwa nini hatuwatendei kama wanavyotutendea? Mwenyezi Mungu anasema { **Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.**} Mumtahina:8.

Wema ni neno lenye kukusanya maana zote za kheri, upendo, hisia nzuri, pia uadilifu ambao kwa ajili yake mbingu na ardhi zimesimama.

Ulinzi wa makanisa katika uisilamu²⁵

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema mwenye Kurehemu

{1. Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye amemteremshia mja wake Kitabu, wala hakukifanya kina upogo. 2. Kimenyooka sawa, ili kitoe onyo kali kutoka kwake, na kiwabashirie Waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri.} Kahf:1-2.

Rehema na amani zimshukie aliyetumwa kuwa ni Mtoa bishara na Mtoa maonyo na Mlinganiaji wa Mwenyezi Mungu kwa uwezo Wake na ni mwanga wenye kuangaza. Dalili akaziweka wazi, akaondosha ujinga, Muhammad bwana wa Mitume na kiongozi wa wamchao Mungu, na kwa jamaa zake na Masahaba wake watukufu.

Baada ya utangulizi.

Kitu kisichofichikana ni kuwa kuna mikono ya chini kwa chini (iliyojificha), ambayo ina chochote fitina kati ya waisilamu na wakiristo, kwa nyakati tofauti, kwa kutumia nafasi za wenye misimamo mikali kwa baadhi ya wakati, na nyakati nyengine hutumia mwenye wa ujinga wa watu.

Hili linaonekana wazi kwa yale matokea ya kiuadui la makundi ya wenye misimamo mikali kuyahujumu makanisa katika baadhi ya nchi za kiisilamu ulimwenguni. Kama wafanyavyo kundi la wapiganaji wa dola la Kiisilamu (IS) nchini Syria, Iraq, na nchi nyenginezo kwa kubomoa, kuunguza makanisa na kuvunja haki. Na kama vile wafanyavyo baadhi ya taasisi za kigaidi nyenginezo na makundi yenye misimamo mikali ambayo huamini yasiyo sahihi. Jambo ambalo huleta wasiwasi katika nyoyo za waisilamu na wakiristo na hupelekea kuzuka kwa ugomvi mkubwa, pengine ni kwa sababu ya kuwepo kwa agenda za siri kutoka nje, zenye kuchochea haya yote. Na kusababisha kuuwasha moto wa fitina kati ya

²⁵ Utafiti huu umeandikwa na Prof; Abdul Halim Mansour. Wakili wa Kitivo cha Sheria na Kanuni – Chuo Kikuu cha Al azhar- Daqahliya.

waisilamu na wakiristo, si hivyo tu bali pengine wanashiriki na kuwa ni viungo katika kueneza mambo haya kwa vijana wa kiisilamu.

Wasimamiao mambo haya yasiyo na maana kutoka pande zote pengine wameshikamana na athari (dalili) zilizo dhaifu ambazo hazifai kutumika katika kutoa hukumu za kisheria, hivyo ni wajibu wa kubainisha hukumu za kisheria kuhusu matendo ya kuhujumu makanisa na maeneo mengine ya ibada za wasiokuwa waisilamu.

Mwanzo tunasema:

Uisilamu unaharamisha vitendo vya kiuadui katika maeneo ya ibada, makanisani, nyumba za watawa, misikitini na sehemu nyengine, ama kwa upande wa hukumu tutasema kama ifuatavyo:-

Kwanza: Uisilamu umedhamini uhuru wa kuabudu

Kitu kijulikanacho na wote ni kuwa, uisilamu umetoa uhuru wa kuabudu kwa watu wote na ukaharamisha kulazimisha katika kuingia katika uisilamu, na haya ni kama ilivyo katika aya {**Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.**} Albaqara:256. na maneno yake Mwenyezi Mungu { **Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?}** **Yunus:99.** aya hizi mbili zinajulisha wazi kuwa hakuna kulazimisha katika kuingia kweney dini ya Mwenyezi Mungu. Na kutokana na uhuru uliopo katika uisilamu wa kuabudu inalazimu pia kwa asiye muisilamu kufanya mambo yote ya dini yake ndani ya maeneo ya ibada na kulazimika kuyalinda.

Pili: Wajibu wa kuyahifadhi maeneo ya ibada

Kwa dalili. Mwenyezi Mungu anasema {**Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia 40. Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka**

zingeli vunjwa nyumba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu.} Alhaji:39-40.

Na dalili ni kuwa:

Mwenyezi Mungu ametaja kuvunjwa kwa nyumba za watawa, makanisa, masinagogi na misikiti katika hali ya kukana na hayo yote yameunganishwa kwa kiunganishi cha “na” hii ikiwa na maana hukumu ya hayo yote inashirikiana na kuwa moja nayo ni kutofaa kuvunjwa kwa makanisa.

Na maneno yake Mtume (rehma na amani zimshukie) “usidhure wala usidhurike”²⁶

Dalili ni kuwa Mtume amekataa kufanya madhara ya kumdhuru mtu na kujidhuru mwenyewe, ikiwa na maana mtu asimdhuru mwengine ili haki yake isije ikapotea na miongoni mwa kupoteza haki ni kumnyima mtu kuabudu sehemu za kuabudia, na hii ni madhara ambayo hayafai kwa mujibu wa sheria.

Tatu: Kutimiza ahadi za wasiokuwa waisilamu

Imezoeleka tangu zama za Mtume (rehma na amani zimshukie) na Masahaba zake na waliowafuata baada yao mpaka sasa kuwa makanisa na masinagogi hayahitajiki kufikwa na mashambulizi.

Makanisa yaliyopo katika eneo la Dar Salaam (mji katika nchi ya Misri) hayapaswi kuvunjwa, kwani yapo tangu zama za zamani na hili hapana shaka kuwa Masahaba

²⁶ Ibn Maajah. 2/784. namba 2340, kutoka kwa Ibn Abbas.

na waliowafuatia baada yao walipofungua mji huo walijua uwepo wake na wakaliacha kama lilivyo.²⁷

Na kama ilivyopokea katika mikataba ya amani ambayo Mtume(rehma na amani zimshukie) na Masahaba zake na waliowafuatilia ni kuwa waliwapa amani wasiokuwa waislamu katika damu zao, mali zao, heshima zao, nyumba zao za watawa, makanisa yao na kutoyaharibu na kuvunja kitu chochote katika hayo. Kwa ushahidi:-

1) Zama za Mtume (rehma na amani zimshukie) ameandikwa kuwaandikia watu wa Najraan. Haya ni katika aliyoyaandika Muhammada Mtume na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu wa Najiran iwapo ana hukumu kwao. kwa watu wa Najirani na majirani zao ni dhima ya Mwenyezi Mungu na dhima ya Mtume wake juu ya miji yao, mali zao, mila zao, kuuziana kwao, Makasisi wao, Maoskofu wao, waliopo miongoni mwao na wasiokuwepo miongoni mwao kuwa wasiwabadilishe Oskofu katika Maoskofu wao, wala Kasisi katika Makasisi wao, na wala wasichukuliwe kwenda kupigana jihadi na wala mali zao za zaka zisichukuliwe fungu la kumi.²⁸

2) Zama za Umar (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) kawaandikia watu wa Qudsi: Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye Kurehemu... Haya ndio aliyoyatoa mja wa Mwenyezi Mungu Umar kiongozi wa waislamu kwa watu wa Ilyaa, kuwapa ulinzi na amani wa nafsi zao na mali zao na makanisa yao na sala zao na mila zao nyengine. Musikae katika makanisa yao wala musiyabomoe wala musipunguze kitu hata kama ni kidogo, hata msalaba wake, na

²⁷ Sharhu fathu Kadiyr. 6/58.

²⁸ Nayli Awtwaar 8/13.

chochote katika mali zao, wala musiwalazimishe juu ya dini yao na wala asidhuriwe yeyote katika hao, wala asijenge Myahudi yeyote katika Iliyaai.”²⁹

3) Amepokea Yaqubiy katika kitabu chake, mkataba ulioandikwa kama ifuatavyo “Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye Kurehemu... Haya ni katika aliyoaandika Umar bin Khatab kwa watu wa Qudsi, nyinyi damu zenu na mali zenu ziko salama, makanisa yenu hayatakaliwa na hayatavunjwa, isipokuwa kama litatokea tukio kubwa na kushuhudiwa na mashahidi.”³⁰

4) Imepokewa na Umar bin Abdul Aziz (Mwenyezi Mungu amwie radhi) kuwa amewaandikia wafanyakazi wake: “Msibomowe nyumba za watawa wala kanisa wala nyumba za waabudiao moto.”³¹

Na hii ni dalili ya wazi kuwa ni wajibu kuheshimu maeneo ya ibada za wasiokuwa waisilamu, bila ya hivyo basi ile mikataba ya Mtume na Masahaba zake ya kuweka usalama katika maeneo hayo haitokuwa na maana yoyote, kwani iweje aweke usalama sehemu ambayo haihitajiki kuwa na usalama? Hivyo haifai kuvunja na kuharibu maeneo hayo.

Nne : kuondosha sababu zinazopelekea uharibifu

Kufanya uadui katika maeneo ya ibada ya wasiokuwa waisilamu na kuharibu mambo wanayoyatakasa hii itapelekea na wao kuivunja misikiti ya waisilamu, na kama ni hivyo, basi kuzuia kuvunja makanisa ndio njia pekee ya kuzuia misikiti nayo isivunjwe. Mwenyezi Mungu anasema {**Wala msiwatukane hao wanao**

²⁹ Taarikh Twabariy. 3/609 Chapa Maarif.

³⁰ Tariykh Yaaqubiy. 3/147.

³¹ Ibn Abi Shaybah 6/467.

waomba badala ya Mwenyezi Mungu, wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua.} Al anaam:108.

Baada ya hayo; Kutokana na mtazamo huu wa haraka wa kubainisha hukumu za kufanya vitendo vya kiuadui katika maeneo ya ibada ya wasiokuwa waisilamu, itafahamika wazi kuwa hakuna aya au hadithi yenye kuruhusu uvunjaji au hata yenye kushajiisha kufanyika kwa vitendo hivyo, lakini kinyume chake ndio sahihi. Aya za Qurani Tukufu na mikataba ya amani aliyoiweka Mtume na Masahaba zake kwa waliopewa kitabu inaonesha kuwa uisilamu unahifadhi na kulinda watu wa dini waliopewa kitabu inawahifadhi damu zao, itikadi zao na makanisa yao. Na historia ya kiisilamu ina mifano mingi ya kuthibitisha jambo hili, na yeyote asema vitabu vya watunzi wa zamani wataona kuwa wanaruhusu kuusia kujengwa kwa makanisa na makanisa wanayoyazungumzia yapo hadi hivi sasa katika miji yetu. Basi kwa nini kunatokea michafuko kama hii, kwa nini watu hawarudi katika usawa wa dini na kuacha siasa kali, Mwenyezi Mungu anasema { **Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia.} Qaaf:37.**

Ulinzi wa makanisa katika Uisilamu³²

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema mwenye kurehemu.

Shukurani zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehema na amani zimshukie Mtume Muhammad na watu wake na Masahaba zake na kila aliyemfuata mpaka siku ya mwisho.

Baada ya utangulizi

Uisilamu ni dini ya kuishi kwa pamoja, na misingi yake haijui kulazimisha, wala fujo, huu ni utangulizi kuhusu dini hii tukufu, ambayo kama itakuwa ndani ya nyoyo yakitoa mmoja wetu basi katu hatokuwa na chuki, Mwenyezi Mungu anasema { **Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uwongofu umekwisha pambanuka na upotofu.**} **Albaqarah:256.** Na anasema {**Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi.Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae**} **Kahf:29.** Na Mwenyezi Mungu anasema { **Nyinyi mna dini yenu, nami nina Dini yangu }** **Alkafiruu:6.**

Kutendana kwa wema na ucha Mungu na usawa.

Mwenyezi Mungu amewaamrisha waisilamu kuonesha wema na upendo na usawa wanapotaamali na wenye itikadi nyengine, akasema { **Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.**} **Mumtahina:8.**

Kwa ajili hiyo, waisilamu waliotangulia wakati wa historia yao nzuri na tabia zao njema ambazo zilipenya na kuingia katika nyoyo za watu ambao waliingia katika miji yao, tangu zama za makhalifa walioongoka mpaka sasa.

³² Utafiti huu umeandikwa na Prof; Majdi Ashuur. Mshauri wa Elimu wa Mufti wa Misri.

Maneno ya Umar bin Al Khatab “ haya ndio aliyoyatoa mja wa Mwenyezi Mungu Umar kiongozi wa waislamu kwa watu wa Ilyaa, kuwapa ulinzi na amani wa nafsi zao na mali zao na makanisa yao na sala zao na mila zao nyengine. Musikae katika makanisa yao wala musiyabomoe wala musipunguze kitu hata kama ni kidogo, hata msalaba wake, na chochote katika mali zao, wala musiwalazimishe juu ya dini yao na wala asidhuriwe yeyote katika hao.” Na kwa haya yaliyomo katika waraka ni ahadi ya Mwenyezi Mungu na dhima ya Mtume wake (rehma na amani zimshukie) na dhima ya viongozi na dhima ya waumini pindi wakipewa wale wenye kutakiwa kulipa kodi. Na hili wameshuhudia Khalid bin Walid, Amru bin Aas, Abdulrahman bin Auf, Muawiyah bin abi Sufyan.³³

Na akaandika waraka kwa watu wa Ludda wenye kufanana na huu, “kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mweny kurehemu, huu ni aliotowa mja wa Mwenyezi Mungu Umar kiongozi wa waumini kwa watu wa Ludda na walioingia pamoja nao katika watu wa Palestina, wapeni usalama wa nafsi zao, mali zao, makanisa yao, misalaba yao, visima vyao na mila zao nyengine: makanisa yao yasikaliwe wala kubomolewa wala wasipunguzwe ndani yake kitu chochote hata kama ni kidogo, wala msalaba wake wala mali zake, wala musiwalazimishe katika dini yao na wala asidhuriwe yeyote.³⁴

Na alipoingia Umar (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) nyumba tukufu ya Qudusi ukakaribia wakati wa sala naye yumo ndani ya kanisa, akasema kumwaambia Askofu: “ninataka kusali” akaambiwa: “Sali hapo ulipo, hakusali pale alipo na akasali peke yake katika ngazi iliyopo nje ya mlango wa kanisa.

³³ Taariykh Twabariy 2/449. chapa Dar Elmiyah.

³⁴ Taariykh Twabariy 2/449. chapa Dar Elmiyah.

Alipomaliza sala akamwambia askofu: “Ningelisali ndani ya kanisa waisilamu baada yangu wangelilichukua na kusema Umar alisali sehemu hii.³⁵”

Na wamagharibi wamelichukua tukio hili kwa mshangao mkubwa sana kama alivyofanya Darmunghim katika kitabu chake “Maisha ya Muhammad (rehma na amani zimshukie). Na Qurani na Hadithi za Mtume zima mifano mingi sana yenye kuonesha usamehevu. Na wafunguzi wa kiisilamu walifuata nyayo za waliowatangulia kwa umakini zaidi. Wakati Umar alipoingia Qudusi alitoa maagizo kwa waisilamu kuwa wasiwasababishie wakiristo au makanisa yao matatizo yoyote. Na alipoitwa na kiongozi wa kikiristo kufanya ibada ndani ya kanisa alijizuia na kutoa sababu ya kuwa, pindi angeliingia na kusali ndani ya kanisa basi waisilamu wangeliwashinda wakiristo na kufanya kuwa ni sehemu yao.³⁶

Na mfano kama huu Khalid bin Waliyd aliwapa usalama na amani watu wa Damuscus kwenye makanisa yao na akawaandikia pia.³⁷

Na mfano mwingine unaofanana na huu, Sharhabiyil bin Hasan (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) amewaandikia watu wa Twabariya, akawapa usalama wa nafsi zao na makanisa yao.³⁸

Vilevile wamefanyiwa watu wa Humus na watu wa Halab.³⁹ Iyaadh bin Ghannam (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) kawaandikia watu wa Riqa kupewa usalama wa nafsi zao na usalama wa makanisa yao na akawaandikia mkataba.⁴⁰

³⁵ Tariykh Ibn Khaldun. 2/225. chapa Dar Ihyaa turath alaraby

³⁶ Tasamuh Wal adawa bayna L islaam Walgharb. Salih Husein. 120-121.

³⁷ Angalia. Futuuhu Albuldaan. Uk 30.

³⁸ Futuuhu Albuldaan. Uk 115.

Namna hiyo hiyo amefanya Habib bin Muslima (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) kwa watu wa Dabiyl, ni mji uliopo Urminia, akawapa amani wa nafsi zao, mali zao, maknisa yao na nyumba za watawa wao wa kiyahudi na kinasara na waabudiao moto, waliokuwepo na wasiokuwepo, akawaandikia mkataba, na hayo yalikuwa katika zama za uongozi wa Othman bin Affan (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie).⁴¹

Imepokewa kutoka kwa Ubayya bin Abdallah Anaghayy amesema: “Umar bin Abdul aziz (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) alituletea barua kuwa “musibomowe nyumba za watawa, wala kanisa, wala nyumba za waabudiao moto
42

Kutoka kwa Atwaa (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) aliulizwa: “je makanisa hubomolewa? Akasema“hapana” isipokuwa yaliyomo ndani ya Haram.⁴³

Na ilipotokezea matatizo katika mikataba hii ikarudishwa kwa kiongozi na kuifanyia marekebisho kasha ikarudishwa tena kwa weneyewe: imepokewa kutoka kwa Ali bin Abi Himlah amesema; tuliwashitaki wageni wa Damuscus kwa Umar bin Abdul Aziz (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) kuhusu kanisa ambalo mtu Fulani alilifanya kuwa ni la bani Nasri nchini Damascus, Umar akatutoa ndani ya kanisa hilo na kuwarudishia (wenyewe) Manasara.⁴⁴

³⁹ Futuuhu Albuldaan. Uk 130-146.

⁴⁰ Futuuhu Albuldaan. Uk 172.

⁴¹ Futuuhu Albuldaan. Uk 199.

⁴² Al amwaal, Abi Ubaydi Alqasim bin Salaam. Dar Fikr. Uk 123.

⁴³ Ibn Abi Shaybah. Namba 32984.

⁴⁴ Al amuwaal 201.

Uharamu wa kuyafanyia uadui makanisa kwa namna yoyote

Uisilamu ulipowaachilia watu uhuru wa dini na kuwaruhusu kuabudu kupitia dini zao kama watakavyo na kudhamini usalama katika maeneo ya ibada; pia ukaharamisha vitendo vya uharibifu na uadui kwa namna zote. Na Qurani Tukufu ikaeleza kuwa sababu ya kufanikiwa kwa waisilamu katika jihadi zao ni kwa kule kuondoa dhuluma na uadui kitu ambacho Mwenyezi Mungu akawapa ushindi katika ardhi na kuweza kuhifadhi maeneo ya ibada na kuyafanya kuwa yawe salama pamoja na watu wake, Mwenyezi Mungu anasema kuhusu hili { **Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa nymba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu. 41. Wale ambao tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Sala, na wakatoa Zaka, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya. Na kwa Mwenyezi Mungu ndio marejeo ya mambo yote.} Alhadjj40-41.**

Anasema Muqatil bin Sulayman: “watu wa mila hizi zote wanamtaja Mwenyezi Mungu ndani ya nyumba zao za ibada, Mwenyezi Mungu akawapa hifadhi kutoka kwa waisilamu.⁴⁵

Anasema imamu Kurtubiy: “lau kuwa Mwenyezi Mungu hakuwaruhusu Mitume kupigana kwa ajili ya kujikinga na maadui zao basi washirikina wangelitawala na

⁴⁵ Tafsir Muqatil Bin Suleyman, 2/285. chapa Dar Al kutub El ilmiyah.

kuondosha majengo yote ya ibada ya dini yengine, lakini ameweka ulinzi kwa kuwajibisha kujikinga na maadui ili wenye dini wapate kufanya ibada zao.

Na imepokewa kutoka katika hadithi ya Mtume (rehma na amani zimshukie) kuwa amemwandikia Askofu wa Bani harith bin Kaab na Askofu wa Najraan na makasisi wengine: “ wanayo yale wanayoyamiliki mikononi mwao sawa iwe ni ndogo na kubwa katika nyumba za ibada, na sala zao, na utawa wao, na ujirani na Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani zimshukie), na mimi simbadilishi askofu na uaskofu wake, na wala kasisi na ukasisi wake, na wala sibatilishi haki miongoni mwa haki, na wala sibatilishi chochote katika vile walivyokuwa navyo, kusuluhisha na kutengeneza ni kwao weneywe, bila ya kufanya dhuluma na wala kudhulumiwa.”⁴⁶

Hivyo, itabainika wazi kuwa kuvunja makanisa au kuyaripua au kuua waliomo ndani yake au hata kuchochea watu wake katika yale yasiyofaa ni mambo yaliyoharamishwa ambayo hayamo ndani ya sheria tukufu. Hayo ni katika mambo yanayokatazwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mtendaji wa haya atakuwa ni hasimu wa Mtume (rehma na amani zimshukie) siku ya kiyama.

Kutekeleza ahadi za utaiifa

Hapana shaka kuwa kuyafanyia uadui makanisa na wakiristo nchi Misri na kokote kule duniani ni kuvunja ahadi ya utaiifa (uzalendo), kwani wao ni wananchi na wana haki, na wameekeana ahadi na waislamu za kuishi kwa pamoja na kwa salama. Kuwafanyia uadui au kuwabughudhi na kumwaga damu zao au kubomoa na kuvunja makanisa yao kuna uteguaji wa ahadi na kupoteza dhima wa waislamu kitu ambacho kimekatazwa na aya za Qurani pia mienendo ya Masahaba. Mwenyezi Mungu anasema { **Enyi mlio amini! Timizeni ahadi**} **Al maidah:1.**

⁴⁶ Ameitoa Abu Ubaydi Alqassim bin Salaam, kitabu cha Al amuwaal. Uk 244. Chapa. Dar Maarifah.

Imepokewa na imam Bukhari katika kitabu chake kutoka kwa Abdalla bin Amru (radhi za Mwenyezi Mungu ziwashukie) kuwa Mtume (rehma na amani zimshukie) anasema: “ Mambo manne mwenye kuwa nayo huwa ni mnafiki wa kweli, na mwenye kuwa na chembe yake basi huwa na chembe ya unafiki mpaka aliache; akiaminiwa hatimizi, akizungumza hudanganya, akiahidiwa huvunja ahadi na akigombana basi huvuka mipaka.⁴⁷

Na katika mapokezi: “Pindi mtu atakuwa yupo katika amani ya nafsi yake kasha akamuua (mwengine) basi mimi niko mbali na muuaji na hata kama aliyeuliwa ni kafiri.”⁴⁸

Na kutoka kwa Ali (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) Mtume wa Mwenyezi Mungu (rehma na amani zimshukie) amesema ‘ Dhima (ahadi) ya waisilamu ni moja wanakuwa nayo hadi mdogo wao basi mwenye kuikengeuka laana za Mwenyezi Mungu na malaika na watu wote ni juu yake, na hatakubaliwa matendo wala amali⁴⁹.(hatokubaliwa matendo yake yoyote, ya faradhi au ya sunna).

Pia haifichikani kuwa, kutoyalinda makanisa na kinyume chake kuwatishia watu wake, ni katika kuvunja ahadi na kuwakera wananchi. Imepokewa kutoka kwa Abi Hurayra (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) amesema: amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu:“Muumini haiwezikani kusambaratika imani yake hata kidogo “ maana ya hadithi ni kuwa; imani inazuia mtu kusambaratika kama inavyozuia pingu mtu kutoweza kufanya atakalo.”

Mtume (rehma na amani zimshukie) amewausia watu wa Misri wasia maalumu, akasema kutoka kwa mama wa waumini Ummu Salama (radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie) kuwa Mtume (rehma na amani zimshukie) ameusia wakati wa

⁴⁷ Bukhari na Muslim.

⁴⁸ Ameitowa Bayhaqiy. Sunanu L kubraa. Nambari 18422.

⁴⁹ Ameitowa Bukhari. Nambari 1870.

kufariki kwake, akasema; “ tahadharini tahadharini na Waqibti wa Misri, nyinyi mtakwenda kwao na watakupokeeni na ni wasaidizi katika njia ya Mwenyezi Mungu.”⁵⁰

Imepokewa kutoka kwa Mussa bin Jubayr, kutoka mashehe wa watu wa madina: kuwa Umar Bin Al-khatwab (radhi za Mwenyezi Mungu) amemwandikia kiongozi wa Misri Amru bin Aas (radhi za Mwenyezi Mungu) elewa ewe Amru kuwa Mwenyezi Mungu anakuona na anaona matendo yako Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema { **na tukawafanya wacha Mungu kuwa ndio viongozi** } akikusudia; kuwa ndio wafuatwe. Na unao watu wa dhima na wa ahadi na Mtume (rehma na amani zimshukie) amewausia Maqibti akasema: “ wausieni Waqibti kheri, kwani wana dhima na rehema (upendo). Na Mtume (rehma na amani zimshukie) amesema: “Mwenye kumdhulumu mtu wa dhima au kumkalifisha zaidi ya uwezo wake basi mimi nitakuwa kinyume naye (hasimu yake) siku ya kiyama.” Jihadhari ewe Amru kuwa Mtume yuko mbali nawe (hasimu yake), kwani mwenye kuwa mbali naye basi atakuwa mbali mno.⁵¹

Na mwenye kuangalia historia ataona ukweli wa maneno ya Mtume (rehma na amani zimshukie) kwa namna alivyowakaribisha Maqibti wa Misri kwa waisilamu waliofungua na wao wakawafungulia nyoyo zao. Na wakaishi nao kwa amani na usalama. Na kuifanya Misri kuwa ni jaribio kubwa la historia iliyojaa mafanikio ya kuishi kwa pamoja na kushirikiana ndani ya nchi moja baina ya raia zake kama sheria inavyosema.

Na kwa kuwa kuna ulazima wa kuhifadhi mambo matano ambayo mila zote zimekiri kuyahifadhi nayo ni;- dini, nafsi, akili, heshima na mali kwa kuwa haya ndio mambo ya msingi wa kila sheria.

⁵⁰ Imetolewa na Twabari. Muujam kabiyr. Namba 561.

⁵¹ Angalia; Kanzu L umaal. Lil mutaqiy Al hindiy. 5/760.

Na baadhi ya waovu wanapinga haya makusudio matano ya kisheria ambayo ni lazima yalindwe na kuhifadhiwa, mfano kuhifadhi nafsi, anayeuliwa huwa ni raia asiyejua hili wala lile na ana nafsi ambayo ni lazima ilindwe isiyohitaji kufanyiwa uadui. Mwenyezi Mungu ameipa nafsi ya mwanadamu nafasi ya juu kabisa akasema { **aliye muuwa mtu bila ya yeye kuuwa, au kufanya uchafuzi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote. Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote. }Almaidah:32.**

Kwa ajili hii, uharibifu wa nafsi ni katika uufisadi mkubwa, kwani kuna sura mbaya inajengeka katika akili za watu wa mashariki na magharibi kwa kuwapa picha isiyo sahihi ambayo maadui wa uisilamu wanaidhirisha ulimwenguni kuwa uisilamu una kiu ya damu nalo ni neno lisilo na ukweli ndani yake. Kwa njia hii maadui wengi wamepitia njia hii kwa ajili ya kusema mambo ya ndani ya uisilamu bila ya haki.

Mwenyezi Mungu ameamrisha kuacha sababu za kupelekea kuwatusi wengine ili wasije kumtusi Mwenyezi Mungu. Anasema { **Wala msiwatukane hao wanao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua. Namna hivyo tumewapambia kila umma vitendo vyao. Kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao Mlezi, naye atawaambia waliyokuwa wakiyatenda.} Al anaam:108.**

Amesema imamu Raziyy, “ aya hii inajulisha kuwa makafiri hawatakiwi kutendewa kile ambacho kitazidi kuwaweka mbali na ukweli na kuwazidishia inadi, na kama itafaa basi ingefaa kuamrisha, na Mwenyezi Mungu anaamrisha upole wakati wa ulinganio kama mfano wa Mtume Mussa na Harouna (rehma na amani ziwashukie) {**Mukamwambie maneno laini huenda akakumbuka au akaogopa**}⁵²

⁵² Mafatihul Ghayb. Dar Elkutub.13/115.

Ufupisho

Uisilamu unahifadhi haki za wengine na ni miongoni mwa maisha ya ukarimu kati ya waislamu, hivyo hivyo kuhifadhi maeneo ya ibada na kuyalinda kutokana na vitisho vya aina yoyote vyenye kuvunja amani kwa raia. Na hapana shaka kuwa hukumu za kisheria pia zinatumiwa katika sheria zilizopo za kisasa. Kwa kwenda sambamba na misingi ya kuishi kwa pamoja na kutimiza ahadi za uzalendo ambazo zinamuhusu kila mtu sawa awe muisilamu au dini nyengine, chini ya kivuli cha kanuni moja, yenye kuwaweka sawa wote na wenye kutimiza majukumu yao na kazi zao za kuimarisha nchi kwa usawa na haki. Ili kila mmoja ahisi nafasi yake ndani ya taifa, na washiriki katika Nyanja tofauti katika kutoa uwezo wao na vipaji vyao na ujuzi walionao kwa lengo la kuimarisha ujenzi wa taifa katika sekta mbalimbali.

,,,,, mwisho wa maneno yetu ni shukurani zote ni za Mola wa walimwengu,,,

№	Maudhui	Ukurasa
1	Utangulizi Profesa; Muhammad Mukhtar Juma Waziri wa wakfu	2
2	Utangulizi Profesa; Shauky Allaam Mufti wa Misri	6
3	Ulinzi wa makanisa na athari zake katika kuuonyesha utukufu wa uisilamu Profesa; Muhammad Salim Abu Aas	8
4	Ulinzi wa makanisa katika Uisilamu Profesa; Abdallah Najar	12
5	Ulinzi wa makanisa katika Uisilamu Profesa; Muhammad Aljabal	15
6	Ulinzi wa makanisa katika Uisilamu Profesa; Muhammed nabil Alghanam	17
7	Ulinzi wa makanisa katika Uisilamu Profesa; Abdallah Alhalim mansour	20
8	Ulinzi wa makanisa katika Uisilamu Profesa; Magdi Ashuur	23
9	Yaliyomo	40